



UnapojibuTafadhalitaja:
Kumb Na: NTC/E:P/152/1B/04

16/06/2026

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MKATABA WA MUDA WA MWAKA MMOJA (1) YA UKAGUZI WA MAPATO KWENYE MAGETI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Njombe anawatangazia nafasi 75 za kazi za Mkataba wa Muda wa mwaka mmoja (1) ya Ukaguzi wa Mapato Magetini na anakaribisha maombi kwa watanzania wote wenye sifa na uwezo kwa ajili ya kujaza nafasi ya kazi kama ilivyo orodheshwa katika tangazo hili. Aidha mnajulishwa kuwa mwisho wa maombi haya ni tarehe **30/06/2026**.

1. MKAGUZI WA MAGETINI - NAFASI 75

(a) Sifa za mwombaji.

Mwenye elimu ya kidato cha nne au sita, aliyefaulu somo la Hisabati.

Kazi na majukumu

- a) Kuhesabu na kuhakiki ili kujiridhisha kuwa mzigo uliopakiwa kwenye chombo cha usafirishaji umelipiwa ushuru wa Halmashauri na unastakabadhi halali ya Serikali inayolingana na tozo stahiki.
- b) Kutunza Kumbukumbu za magari yote yaliyobeba mazao ya misitu, mazao ya biashara na chakula yanayopita kwenye kizuizi (geti) cha Halmashauri.
- c) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata na Mtendaji wa Kijiji ambapo geti lipo na kwa Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Njombe.

2. MAELEKEZO

- i. Waombaji wote wawe raia wa Tanzania wasiozidi umri zaidi ya miaka 45 na wasiopungua umri wa miaka 18.
- ii. Waombaji wote waombe kwa kufuata masharti ya TANGAZO LA KAZI,
- iii. Waombaji lazima waambatanishe nakala za vyeti vifuatavyo:-
 - a) Cheti cha mtihani wa kidato cha nne au sita.
 - b) Cheti cha kuzaliwa.
 - c) Picha mbili za passport size za hivi karibuni.

hazitafanyiwa kazi.

- v. Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au kingereza.
- vi. Watakaoitwa kwenye usaili watajigharamia wenyewe.
- vii. Mwombaji anatakiwa kuwa na wadhamini wawili ambao ni watumishi wa Umma.
- viii. Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe **30/06/2026** saa **9:30** alasiri, baada ya tarehe hiyo kupita maombi hayatapokelewa na watakao chaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili kupitia tovuti ya Halmashauri www.njombe.tz na kwenye mbaao za matangazo za Halmashauri.

NB: Tangazo hili linasahihisha tangazo lenye Kumb.

Na.NTC/E:P/152/1B/03 tarehe 15/06/2026

Barua zote zitumwe kwa:-

MKURUGENZI,
HALMASHAURI YA MJI NJOMBE,
S.L.P 577,
NJOMBE.

Tangazo hili limetolewa na:-


K.A.SADICK
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
NJOMBE.
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
S. L. P 577, NJOMBE